



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Iringa

Novemba 09,202

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII AMEFUNGUA MAONESHU YA UTALII KUSINI**

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amefungua rasmi maonesho ya Karibu Utalii Kusini 2022 yanayoendelea Leo Novemba 09 hadi Novemba 13, 2022 katika Mkoa wa Iringa.

Wakati akiongea na watazania waliofika katika viwanja vya maonesho vya Kihesa Kilolo amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa maono makubwa ya kuibeba sekta ya Utalii nchini si tu kwa Filamu ya The Royal Tour bali kupitia miradi na programu mbalimbali ya Utalii.

Maonesho hayo yamehusisha Mikoa ya Kusini ikiwemo Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Mtwara, Lindi, Songwe, Mbeya, na Morogoro.

Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa mikoa ya kusini iliyoshiriki kikamilifu kwenye maonesho hayo ikiwa ni pamoja na kuonesha vivutio vya utalii kutoka kwenye Halmashauri zote za Mkoa wa Njombe.

Viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Njombe, Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias wameshiriki maonesho hayo yanayoendelea.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.**